

Jinsi ya kupiga kura kwa posta



Mwongozo rahisi wa kusoma



Jinsi ya kutumia mwongozo huu




Tume ya Uchaguzi ya Australia (AEC) iliandika mwongozo huu. Wakati unapona neno 'sisi', linamaanisha AEC.



Tumeandika mwongozo huu kwa njia rahisi ya kusoma.

Tunatumia picha kueleza mawazo mengine.



Tumeandika maneno kadhaa kwa **herufi nzito**. Tunaeleza maana ya maneno haya. Kuna orodha ya maneno haya kwenye ukurasa 31.



Unaweza kuomba msaada wa kusoma mwongozo huu.

Rafiki, mtu wa familia au mtu msaidizi anaweza kukusaidia.

Ni nini katika mwongozo huu?

Kupiga kura katika uchaguzi	4
Kujiandikisha kupiga kura	6
Unahitaji kupiga kura lini?	7
Vipi kama huwezi kupiga kura siku ya uchaguzi?	8
Je, unaomba kupiga kura ya posta jinsi gani?	10
Utapata karatasi zako za kura lini?	16
Unafanya nini na karatasi zako za kura?	17
Unajazaje karatasi yako kijani ya kura?	20
Unajazaje karatasi yako nyeupe ya kura?	22
Utaweka karatasi zako za kura wapi?	26
Je! Unahitaji kuomba kupiga kura ya posta kila uchaguzi?	27
Je! Unaweza kujizoea kupiga kura kabla ya uchaguzi?	29
Unawezaje kupata habari zaidi?	30
Orodha ya maneno	31
Wasiliana nasi	34

Kupiga kura katika uchaguzi



Hapa Australia tuna **uchaguzi wa serikali ya shirikisho** karibu kila miaka 3.



Uchaguzi wa shirikisho ni kwa nchi nzima.



Ni jinsi tunavyochagua serikali ya Australia.



Gavana Mkuu anachagua tarehe ya uchaguzi.

Siku ya uchaguzi itakuwa Jumamosi.



Siku hiyo, watu wa Australia **watapiga kura**.

Wakati unapopiga kura, unasaidia katika kuchagua ni nani ambao ni sehemu ya serikali ya Australia.



Unapaswa kupiga kura ikiwa wewe:

- ni **raia** wa Australia na
- una umri wa miaka 18 au zaidi.



Raia ni mtu anayepewa haki na uhuru wa nchi anapoishi.




Kupiga kura kunakupa nafasi kutoa maoni yako juu ya nani wataongoza nchi yetu.

Kujiandikisha kupiga kura



Kabla ya kupiga kura, unapaswa **kujiandikisha**.



Unaweza kusoma mwongozo wetu ambao unakuambia jinsi ya kuandikisha – *Jinsi ya kujiandikisha kupiga kura*.

Unahitaji kupiga kura lini?



Gavana Mkuu anachagua tarehe ya uchaguzi.



Tutaambia watu tarehe ya uchaguzi itakapochaguliwa.



Ikiwa unataka kujua siku ya uchaguzi ni lini, unaweza:

- kutembelea tovuti yetu www.aec.gov.au
- kuuliza mtu wa familia, rafiki au jirani
- tazama Habari kwenye TV
- tafuta mtandaoni
- utupigie simu kwenye **13 23 26**.



Siku ya uchaguzi, kupiga kura hufungua saa 2 asubuhi (8am).



Siku ya uchaguzi, kupiga kura hufunga saa 12 jioni (6pm).



Unapaswa kupiga kura kabla ya kufunga kupiga kura.

Vipi kama huwezi kupiga kura siku ya uchaguzi?



Wakati mwingine, watu hawawezi kupiga kura siku ya uchaguzi.




Hii inaweza kuwa kwa sababu wanaenda likizo.



Au labda watakuwepo hospitalini.



Ikiwa huwezi kupiga kura siku ya uchaguzi, unaweza kupiga kura kabla ya uchaguzi.



Unaweza kutuma kura yako kwa posta.

Hii inaitwa **kura ya posta**.



Unapaswa kuomba kupiga kura kwa posta.



Tunaeleza jinsi ya kupiga kura kwa posta kwenye ukurasa 20.



Unaweza pia kupiga kura katika **mahali kadhaa pa kupiga kura** kabla ya siku ya uchaguzi.



Mahali pa kupigia kura ni jengo, kama vile shule au kituo cha jamii, ambapo watu huenda kupiga kura wakati wa uchaguzi.



Ikiwa unatupigia simu, tutakusaidia kupata mahali pa kupiga kura karibu yako.

13 23 26

Je, unaomba kupiga kura ya posta jinsi gani?



Unaomba kupiga kura ya posta kwa kujaza fomuu.

Tunaita hii ombi la kura ya posta.

Unaweza kujaza ombi la kura ya posta:



- mtandaoni
- kwenye karatasi.

Kujaza ombi lako la kura ya posta mtandaoni



Wakati tarehe ya siku ya uchaguzi imechagua, tembelea tovuti yetu.

www.aec.gov.au/pva



Unahitaji kujibu maswali kadhaa.



Tunaeleza maswali haya kwenye ukurasa 14.



Unaweza kuomba msaada wa kujaza ombi lako la kura ya posta mtandaoni.

Submit

Unapomaliza, unahitaji kutumia kitufe kinachosema: Submit (Peleka).

Kujaza ombi lako la kura ya posta kwenye karatasi



Unaweza kupata fomu ya ombi la kura ya posta kwa ofisi yoyote ya AEC.



Ikiwa unatupigia simu, tunaweza kutuma fomu kwako kwa posta.

Nambari yetu ya simu ni **13 23 26**.



Unahitaji kujibu maswali mengine kwenye fomu.



Tunaeleza maswali haya kwenye ukurasa 14.



Unaweza kuomba msaada wa kujaza ombi lako la kura ya posta kwa karatasi.



Wakati unapomaliza, unahitaji kurudisha fomu kwetu.

Unaweza:



- Kuituma kwetu:

AEC

Reply Paid 9867

Katika mji mkuu wako

Hakuna haja kutumia stempu.




- ichukue kwa ofisi ya AEC

Ikiwa utatupigia simu, tunaweza

kukusaidia kupata ofisi ya AEC karibu


nawe.

13 23 26



- ichanganue na kuipakia kwenye tovuti yetu.

www.aec.gov.au/pva



Maswali kwenye fomu ya ombi la kura ya posta



Swali moja litakuuliza kwa anwani yako.



Unapaswa kutumia anwani ile ile uliyotupa wakati ulijiandikisha kupiga kura.



Swali lingine litakuuliza **kutuma wapi karatasi zako za kura.**

Karatasi za kura ni fomu ambazo utajaza kuonyesha unataka kupiga kura kwa nani.




Unaweza kutupa:

- anwani unapoishi
- anwani nyingine ya kutuma posta yako yote
- anwani ambayo utatembelea katika
 - jimbo lingine
 - nchi nyingine.



Tutakuuliza swali la usalama.

Hili ni kama neno la siri.



Unaweza:

- kuchagua swali lako la salama
- kuandika jibu lako lenyewe.



Unahitaji kukumbuka jibu lako.



Labda utapenda kuliandika na kulitunza salama.

Utapata karatasi zako za kura lini?




Tutatuma karatasi zako za kura kwako wakati wa kupiga kura.



Utapata hizi katika posta.

Utapewa:



- Karatasi 2 za kura:
 - ya nyeupe
 - ya kijana



- bahasha ya kura ya posta ili kuweka karatasi zako za kura ndani na kutuma kwetu.

Unafanya nini na karatasi zako za kura?



Kabla ya kuweza kupiga kura, unahitaji kupata **shahidi**.



Shahidi ni mtu ambaye anakujua, kama:

- mtu wa familia
- rafiki
- jirani.



Shahidi wako anahitaji kuwa kwenye rejesta ya wapiga kura.



Shahidi wako anahitaji kuhakikisha kuwa unajaza karatasi zako za kura.



Onyesha karatasi zako za kura na bahasha yako ya kura ya posta kwa shahidi wako kabla ya kuzijaza.



Bahasha ya kura ya posta itakuwa na jina lako na anwani yako.



Pia itauliza swali lako la usalama.



Unahitaji kuandika jibu lile lile kwa swali la usalama ambalo umetoa kwenye ombi lako.



Baada ya hapo, unahitaji:

- kusaini jina lako
au
- kuandika alama yako.



Unaweza kumuuliza shahidi wako kukusaidia.



Unapomaliza, shahidi wako anahitaji:



- kusaini bahasha
- kuandika tarehe.



Wakati hii imefanywa, upo tayari kupiga kura.

Unajazaje karatasi yako kijani ya kura?



Karatasi yako kijani ni kwa

Nyumba ya Wawakilishi


Nyumba ya Wawakilishi:



- ni moja kati ya nyumba 2 za Bunge la Australia - nyumba ambayo serikali huundwa



- inajumuisha watu 151 waliopigiwa kura na watu wa Australia.



Karatasi yako kijani ya kupigia kura ina:

- orodha ya majina ya wagombea
- sanduku tupu.

1



Chagua mgombea ambaye unataka kumpigia kura zaidi.

Andika 1 kwenye sanduku tupu karibu na jina lake.

2




Chagua mgombea ambaye unataka kumpigia kura wa kufuata.


Andika 2 kwenye sanduku tupu karibu na jina lake.



Endelea kuchagua wagombea na kuandika nambari hadi sanduku zote zimejazwa.



Wagombea wengine wanaweza kuwa na maneno au picha karibu na majina yao.



Kila sanduku linapaswa kuwa na nambari tofauti ndani yake.



Wakati kila sanduku limejaa, karatasi yako ya kura imekamilika.

Unajazaje karatasi yako nyeupe ya kura?



Karatasi yako nyeupe ya kura ni ya Seneti.

Seneti:



- ni 1 ya nyumba 2 za Bunge la Australia - inajulikana kama nyumba ya juu
- inajumuisha watu 76 waliopigiwa kura na watu wa Australia kuwakilisha kila moja ya:
 - majimbo 6
 - wilaya 2.



Karatasi yako nyeupe ya kura ina mstari mweusi juu yake.



Kuna orodha ya vikundi juu ya mstari mweusi.

Makundi mengi ni **vyama vya siasa**.



Chama cha siasa ni kikundi cha wagombea ambao:

- wanashiriki maoni sawa
- wanakubaliana juu ya jinsi serikali inapaswa kuendesha nchi yetu.



Kuna orodha ya wagombea chini ya mstari mweusi.

Kuna njia 2 za kujaza karatasi nyeupe yako ya kura:

3 1 2



- weka nambari kwenye visanduku hapo juu ya mstari mweusi na upigie kura kwa vikundi

au



- weka nambari kwenye visanduku chini ya mstari mweusi na upigie kura wagombea.

Kupiga kura juu ya mstari mweusi



Chagua kikundi unachotaka kupiga kura zaidi.
Andika 1 kwenye sanduku tupu karibu na jina lake.




Chagua kikundi unachotaka kupiga kura ijayo.
Andika 2 kwenye sanduku tupu karibu na jina lake.


3 1 2



Endelea kuchagua vikundi na kuandika nambari hadi visanduku 6 zimejazwa.
Unaweza kumaliza kwa 6 au kuendelea.



Ikiwa kuna chini ya sanduku tupu 6, weka nambari katika kila sanduku.



Makundi mengine yanaweza kuwa na maneno au picha karibu na majina yao.

Kupiga kura chini ya mstari mweusi



Chagua mgombea ambaye unataka kumpigia kura zaidi.

Andika 1 kwenye sanduku tupu karibu na jina lake.



Chagua mgombea ambaye unataka kumpigia kura wa kufuata.

Andika 2 kwenye sanduku tupu karibu na jina lake.




Endelea kuchagua wagombea na kuandika nambari hadi sanduku 12 zimejazwa.

Unaweza kumaliza kwa 12 au kuendelea.



Ikiwa kuna chini ya sanduku tupu 12, weka nambari katika kila sanduku.

Utaweka karatasi zako za kura wapi?



Unapokuwa umejaza karatasi zako za kupiga kura, unahitaji kuziweka ndani ya bahasha ya kura ya posta na funga kabisa.



Chukua bahasha ya kura ya posta na weka kwenye sanduku la barua.

Hakuna haja kutumia stempu.



Fanya hii mara moja ili itakuja kwetu haraka.




Unapokuwa umeweka bahasha yako kwenye sanduku la barua basi umemaliza kupiga kura.


Je! Unahitaji kuomba kupiga kura ya posta kila uchaguzi?




Unapaswa kuomba kupiga kura ya posta kabla ya kila uchaguzi.



Lakini unaweza kuomba kuwa **mpiga kura wa posta wa jumla**.



Mpiga kura wa posta wa jumla anatumwa karatasi zake za kura kwa posta kwa kila uchaguzi wa serikali ya shirikisho.



Hii inamaanisha hakuna haja ya kuomba tena kwa uchaguzi mwingine wa serikali.



Unapaswa **kustahili** kuwa mpiga kura wa posta wa jumla.

Ikiwa unastahili, unatimiza mahitaji yetu.



Hii inamaanisha kwamba utapelekwa kura ya posta kwa kila uchaguzi.



Unaweza kupata habari zaidi na kuomba kwenye tovuti yetu.

www.aec.gov.au/gpv

Je! Unaweza kujizoea kupiga kura kabla ya uchaguzi?



Ikiwa unataka kufanya mazoezi ya kupiga kura, unaweza kutembelea tovuti yetu.

www.aec.gov.au/practice




Kura yako ya mazoezi haina hesabu.



Bado unahitaji kupiga kura:

- mahali pa kupigia kura
au
- kwa posta.

Unawezaje kupata habari zaidi?



Ikiwa unataka kujua zaidi kuhusu kupiga kura, tuna miongozo mingine 2 ambayo unaweza kusoma:

- *Jinsi ya kujiandikisha kupiga kura*
- *Jinsi ya kupiga kura kwa mahali pa kupiga kura.*




Unaweza kupata miongozo hii kwenye tovuti yetu.

www.aec.gov.au/assistance



Pia tuna habari kwenye tovuti yetu kwa watu wanaosema lugha zingine nje ya Kiingereza.

Orodha ya maneno



Karatasi za kura

Karatasi za kura ni fomu ambazo utajaza kuonyesha unataka kupiga kura kwa nani.



Raia


Raia ni mtu anayepewa haki na uhuru wa nchi anapoishi.



Maafisa wa uchaguzi

Watu wanaofanya kazi katika mahali pa kupigia kura kwa siku ya uchaguzi.

Ni kazi yao kukusaidia.



Rejesta za wapiga kura

Orodha ya wapiga kura.



Kustahili

Ikiwa unastahili, unatimiza mahitaji yetu.



Kuandikisha

Wakati unapojiandikisha, tunaweka jina lako kwenye orodha ya wapiga kura.




Uchaguzi wa serikali ya shirikisho

Uchaguzi wa shirikisho ni kwa nchi nzima. Ni jinsi tunavyochagua serikali ya Australia.

Mpiga kura wa jumla wa posta

Mpiga kura wa jumla wa posta:

- anatumwa karatasi zake za kura kwenye posta wakati tarehe ya uchaguzi imechaguliwa
- hakuna haja kuomba tena kwa uchaguzi mwingine wa serikali.



Chama cha siasa

Chama cha siasa ni kikundi cha wagombea ambao:


- wanashiriki maoni sawa
- wanakubaliana juu ya jinsi serikali inapaswa kuendesha nchi yetu.



Mahali pa kupiga kura

Mahali pa kupigia kura ni jengo, kama vile shule au kituo cha jamii, ambapo watu huenda kupiga kura

wakati wa uchaguzi.



Kura ya posta

Unatutumia kura yako katika posta.



Kupiga kura

Wakati unapopiga kura, unasaidia kuchagua ni nani ambao ni sehemu ya serikali ya Australia.



Wapiga kura

Watu ambao wanaweza kupiga kura.



Shahidi

Shahidi ni mtu ambaye anakujua, kama:

- mtu wa familia
- rafiki
- jirani.



Shahidi wako anahitaji kuwa kwenye rejesta ya wapiga kura.

Wasiliana nasi

Huduma ya Kitaifa ya Kupeleka Ujumbe (NRS)



Watumiaji wa TTY:

- Simu 13 36 77
- Uliza kwa 13 23 26



Watumiaji wa sema na sikiliza:

- Simu 1300 555 727
- Uliza kwa 13 23 26



Watumiaji wa Kupeleka Ujumbe Mtandaoni:

- Uganisha kwa NRS
- Uliza kwa 13 23 26



Lugha nyingine:

- Simu 1300 720 153



www.aec.gov.au



[/AusElectoralCom/](https://www.facebook.com/AusElectoralCom/)



[@AusElectoralCom](https://twitter.com/AusElectoralCom)



[@auselectoralcom](https://www.instagram.com/auselectoralcom)



Kikundi cha Kupata Habari kiliunda mwongozo huu rahisi ya kusoma kwa kutumia picha za hifadhi na picha maalum.

Picha hizo haziwezi kutumiwa tena bila ruhusa. Kwa maswali yoyote kuhusu picha, tafadhali tembelea

www.informationaccessgroup.com. Taja nambari ya kazi 3035-C

Imeidhinishwa na Kamishna Naibu wa Uchaguzi, Kanberra.